

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA LIWALE**

NANGANDO SEKONDARI,

S.L.P 22,

**LIWALE.**

04/01/2020.

SIMU: 0686 849999 & 0652 960900

JINA LA MWANAFUNZI \_\_\_\_\_

S.L.P\_\_\_\_\_

**LIWALE.**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI NANGANDO KWA  
MASOMO YA KIDATO CHA KWANZA – MWAKA 2021**

**(JOINING INSTRUCTIONS)**

**UTANGULIZI**

Nafurahi kukutaaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza (I) mwaka 2021 katika shule ya sekondari NANGANDO iliyopo kata ya Nangando. Kwa kuchaguliwa kwake kujiunga na masomo ya sekondari katika shule hii, ameipata fursa ya pekee ambayo wengi wameikosa. Hivyo ninakupongeza na kukujulisha kwamba shule itafunguliwa rasmi tarehe 11/01/2021. Hivyo mwanao/mwanafunzi mnatakiwa kuwepo siku hiyo ya ufunguzi wa shule bila kukosa kwani siku hiyo masomo yataanza rasmi.

Mzazi/Mlezi na mwanafunzi mnatakiwa kusoma maelekezo ya barua hii na kujaza sehemu zinazotakiwa kwa umakini, ili kuepuka usumbufu siku za baadaye.

**“NIDHAMU NA WAJIBU HURUTUBISHA TAALUMA (DISCIPLINE AND  
RESPONSIBILITY NURTURES ACADEMIC EXCELLENCE)”** Ndiyo kauli mbiu ya shule hii, tafakari na tumia nafasi hii kwa manufaa yako na Taifa kwa ujumla.

---

**MOMOY, F.L**

**MKUU WA SHULE**

**FOMU NAMBA 01**

## **MAMBO YA KUZINGATIA**

### **1. SARE ZA SHULE**

#### **A. WASICHANA**

- i. Sketi mbili (2) za rangi ya **kijivu (dark grey)**; Sketi iwe ndefu, mshono uwe wa rinda boksi bila mkanda.
- ii. Mashati mawili (2) meupe; Mikono mifupi, kitambaa cha tetron.
- iii. Viatu vyeusi vya ngozi; viwe vya kutumbukiza vyenye kamba (gidamu). Visiwe vya kupanda, ghorofa au kisigino kirefu.
- iv. Soksi nyeupe jozi mbili (2).
- v. Skafu rangi ya kijivu, rangi sawa na kitambaa cha sketi.
- vi. Sweta rangi ya kijivu
- vii. T-shirt
- viii. Hijabu inaruhusiwa ila sio lazima. Kwa yule atakaye vaa hijabu, iwe nyeupe ambayo itavaliwa na sare ya shule. Mitandio hairuhusiwi. Kwa mwenyekuvaa hijabu, avae na nusu kanzu yenye mikono mirefu.

#### **B. WAVULANA**

- i. Suruali mbili (2) za rangi ya **kijivu (dark grey)**; Upana wa suruali chini usipungue inchi 18, suruali iwe na urefu wa kufunika kiatu kwa sentimeta mbili (2).
- ii. Mashati mawili (2) meupe; Mikono mifupi, kitambaa cha tetron.
- iii. Viatu vyeusi vya ngozi; viwe vya kutumbukiza vyenye kamba (gidamu). Visiwe vya kupanda, ghorofa au kisigino kirefu.
- iv. Soksi nyeupe jozi mbili (2).
- v. Tai rangi ya kijivu rangi sawa na kitambaa cha suruali.
- vi. Mkanda mweusi wa ngozi usio na picha, urembo wala maandishi. Utambi hauruhusiwi.
- vii. Sweta rangi ya kijivu
- viii. T-shirt

**KUMBUKA:** Uvaaji wa sare wa mlegezo maarufu kata K, kutochomekea shati, kutofunga mkanda kwa wavulana, kuvalaa sketi fupi, kuvalaa viatu bila soksi na kutovaa tai haviruhusiwi na ni makosa. Sampuli ya rangi ya kitambaa cha sketi na suruali inapatikana shuleni.

Pia T-shirt zinapatikana shuleni kwa gharama nafuu kwa atakaye hitaji; Sare ya T-shirt za shule zitavalia siku ya Jumatano na Ijumaa.

### **2. VIFAA VYA KUJIFUNZIA DARASANI**

- i. Madaftari makubwa (Counter books) yasiyopungua kumi (10) yenye ukubwa wa kuanzia 2 quire na counter book moja la kuanzia 3 quire kwa ajili ya somo la Hisabati (Basic Mathematics).
- ii. Kalamu (Peni) za kutosha za wino bluu/nyeusi, kalamu za risasi (penseli) na rula.
- iii. Mkebe wa vifaa vya Hisabati (Mathematical Set)
- iv. Ream moja ya karatasi A4 kwa ajili ya mitihani ya Wiki, Mwezi, Ujirani mwema na Mhula.
- v. Kamusi ya Kiingereza (dictionary) na kamusi ya Kiswahili.

### **3. VIFAA VYA USAFI NA UTUNZAJI WA MAZINGIRA**

- i. Ndoo ndogo ya ujazo wa lita 10 na panga au fyekeo kwa wasichana.
- ii. Ndoo ndogo ya ujazo wa lita 10 na jembe kwa wavulana.
- iii. Fagio moja la chelewa.

### **4. VIFAA AU NGUO ZA MICHEZO**

Uongozi wa shule unashauri kila mwanafunzi kushiriki katika michezo kwa afya yake ili afanye vizuri katika taaluma, hivyo mwanafunzi anatakiwa awe na vifaa binafsi vya michezo kwa muongozo ufuatao:-

- i. Viatu aina ya raba kwa wote
- ii. Bukta au traki na fulana rangi ya bluu kwa wavulana
- iii. Traki na fulana rangi ya bluu kwa wasichana.

## **FOMU NAMBA 02**

### **A. MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE**

1. Wizi
2. Uasherati, Ubakaji, Ushoga, Ulawiti na Usagaji.
3. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya, kujihusisha na biashara ya madawa yoyote ya kulevya.
4. Makosa ya jinai.
5. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwanafunzi au mwalimu au na mtu ye yote yule.
6. Kuharibu mali ya umma na ya watu wengine kwa makusudi.
7. Kudharau Bendera ya Taifa, Picha ya viongozi wa Taifa, Nembo ya Taifa, Wimbo wa Taifa na Fedha ya Taifa.
8. Kuoa au kuolewa.
9. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule.

10. Kutoa au kushawishi kutoa mimba.
11. Kugoma au kuhamasisha mgomo, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa watu shulenii.
12. Kukataa adhabu halali.
13. Kujiachisha shule mwenyewe.
14. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
15. Kukaa porini wakati wa masomo.
16. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro
17. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
18. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
19. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
20. Pamoja na makosa mengine yanayofanana na hayo.

## **B. KANUNI ZA SHULE**

### **a. NIDHAMU NA HESHIMA**

Kila mwanafunzi anatakiwa kuzingatia yafuatayo:

1. Kusimama na kumsalimu mwalimu au mtu ye yeyote aliywazidi umri anapopita au anapoingia darasani.
2. Kutotumia lugha mbaya, wakati wowote kati yao wenye, kwa walimu na kwa watu wengine.
3. Kuwaheshimu wafanyakazi wote walioko shulenii kama walezi wake.
4. Kushirikiana na kusaidiana na wanafunzi wenzake katika kazi.
5. Kuthamini na kuheshimu kazi za aina zote.
6. Kuwa na kucha fupi zisizopakwa rangi na nywele fupi pia ziwekwe katika hali ya usafi kila wakati, kuvaav mavazi ya heshima.
7. Kuitika mara moja na kukimbilia aliko Mkuu anayekuita.
8. Kuheshimu bendera ya Taifa, picha za viongozi wa serikali, nembo ya Taifa “coat of Arms”, wimbo wa Taifa na fedha za Taifa.
9. Kuheshimu ukumbi wa mikutano, mahali pa kulia chakula, ofisi za shule, mali ya binafsi na mali ya umma.
10. Kusimama katika mstari wakati wa kupokea huduma.
11. Kuwa mfano mzuri wa heshima na tabia njema mahali popote ulipo.
12. Kunyosha mkono juu na asimame anapouliza na kujibu maswali.
13. Kukaa kimya wakati wote anapokuwa darasani, asitoke bila ruhusa ya mwalimu au kiongozi aliye.
14. Kuheshimu na kukubali tofauti za kisiasa, kidini na kiutamaduni zilizopo katika jamii.

15. Ni marufuku kwa mwanafunzi kuleta vifaa vifuatavyo shulenii SIMU au KIFAA CHOCHOTE CHA SIMU, Camera, VYAKULA vya aina yoyote.

#### **b. MAHUDHURIO**

Kila mwanafunzi anatakiwa:

1. Kuhudhuria shule muda wote wa masomo.
2. Kuhudhuria vipindi vyote vya masomo ndani na nje ya darasa.
3. Kuhudhuria katika kazi zote za mikono.
4. Kuhudhuria mikutano ya shule kama baraza la shule, ukaguzi wa usafi, kupandisha bendera ya Taifa, mikutano ya madarasa.

#### **c. MAENDELEO YA MWANAFUZI KITAALUMA NA TABIA**

Shule humkabidhi mzazi au mlezi taarifa za maendeleo ya mwanafunzi kitabia na kitaaluma kila muhula, tafadhalii mzazi au mlezi hakikisha unaipata na kumshauri mwanaao kuhusu maendeleo yake.

#### **d. KUWAHI**

Kila mwanafunzi anatakiwa:

1. Kuthamini muda.
2. Kuwahi kufika shule na kuhesabu namba.
3. Kuwahi katika shughuli zote za shule kama zilivyopangwa katika ratiba ya kila siku.
4. Kufika shulenii kwa tarehe zilizopangwa kufuatana na muhula husika.

#### **e. SARE YA SHULE**

Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa katika sare ya shule wakati wote wa:

1. Masomo darasani
2. Kutoka nje ya shule Kwa shughuli za kishule.
3. Baraza la shule.
4. Kazi za mikono (T-shirt za shule).
5. Michezo (sare za michezo).

#### **f. MIPAKA YA SHULE**

Kila mwanafunzi azingatie mipaka ya shule Kama ifuatavyo:

1. Ni kosa kwa mwanafunzi kutoka nje ya mipaka ya shule bila kibali cha mwalimu wa zamu.
2. Kutotembelea sehemu zifuatazo isipokuwa kwa kibali maalum:
  - i. Chumba cha walimu (staffroom).
  - ii. Ofisi za shule.
  - iii. Maabara.

iv. Jikoni.

**g. UGONJWA**

1. Tafadhalii mzazi au mlezi unatakiwa kufanya uchunguzi wa kina wa Afya ya mwanaao kabla hajarioti shuleni na wakati wa likizo ili kuepuka usumbufu wakati wa masomo.
2. Endapo kutakuwa na tatizo lolote la kiafya mwanafunzi atatakiwa kutoa taarifa kwa mwalimu wa zamu, mwalimu wa darasa, kwa matron wa shule, mwalimu mlezi n.k. mwanafunzi harusiwi kutunza dawa yoyote darasani. Dawa zote zitunzwe kwa matroni au mwalimu wa afya.
3. Mwanafunzi mwenye matatizo lazima aufahamishe uongozi wa shule au Matron wa shule, mara afikapo shuleni.

**h. USAFI**

Kila mwanafunzi azingatie usafi kama ifuatavyo:

1. Usafi wa mwili.
2. Usafi wa mavazi.
3. Kushiriki usafi wa chumba cha darasa anamosomea.
4. Kushiriki usafi wa vyoo kikamilifu.
5. Kushiriki kufanya usafi wa mazingira kikamilifu.

**ANGALIZO KWA MWANAFUNZI**

1. Mwanafunzi haruhusiwi kuandika maandishi katika dawati, meza, viti, vitabu au kwenye kuta za majengo ya shule.
2. Ni kosa kwa mwanafunzi kukutwa na kitu chochote kinachohusisha mapenzi mfano barua, daftari lenye nyimbo za mapenzi n.k.
3. Ni kosa kwa mwanafunzi kupita eneo lisilo na barabara maalumu au kutupa takataka maeneo yasiyo rasmi au kuziona takataka bila kuziondoa, hii ni kwa ajili ya kutunza mazingira ya shule.
4. Mwanafunzi akiharibu samani, majengo au mali za shule, mzazi/mlezi wa mwanafunzi husika atawajibika kulipa gharama za uharibifu husika.

## FOMU NAMBA 03

### TAARIFA BINAFSI (IJAZWE KIKAMILIFU NA IRUDISHWE SHULENI)

1. Jina lako kamili kama lilivyotumika darasa la saba: \_\_\_\_\_

Tarehe ya Kuzaliwa \_\_\_\_\_

2. Jina kamili la baba mzazi/mlezi: \_\_\_\_\_

Kazi yake \_\_\_\_\_

Anwani kamili ya baba mzazi/mlezi \_\_\_\_\_

Namba yake ya simu ya mkononi \_\_\_\_\_

Mahali anakoishi baba mzazi/mlezi: Tarafa \_\_\_\_\_

Kijiji/Mtaa \_\_\_\_\_

Namba ya Kitambulisho cha Taifa (Namba ya NIDA) \_\_\_\_\_

3. Jina kamili mama mzazi/mlezi \_\_\_\_\_

Kazi yake \_\_\_\_\_

Anwani kamili ya mama mzazi/mlezi \_\_\_\_\_

Namba yake ya simu ya mkononi \_\_\_\_\_

Mahali anakoishi mama mzazi/mlezi: Tarafa \_\_\_\_\_

Kijiji/Mtaa \_\_\_\_\_

Namba ya Kitambulisho cha Taifa (Namba ya NIDA) \_\_\_\_\_

4. Jina kamili la mlezi mwingine mbali na baba mzazi/mlezi au mama mzazi/mlezi \_\_\_\_\_

Uhusiano wa mlezi na mwanafunzi \_\_\_\_\_

Kazi yake \_\_\_\_\_

Anwani kamili ya mlezi \_\_\_\_\_

Namba yake ya simu ya mkononi \_\_\_\_\_

Mahali anakoishi mlezi: Tarafa \_\_\_\_\_

Kijiji/Mtaa \_\_\_\_\_

Namba ya Kitambulisho cha Taifa (Namba ya NIDA) \_\_\_\_\_

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA HALMASHAURI YA**  
**WILAYA YA LIWALE**  
**SHULE YA SEKONDARI NANGANDO**  
**FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE HII**

**1. Sehemu ya mwanafunzi**

**A. KUJIUNGA NA SHULE HII**

Mimi ..... ninakubali nafasi  
niliyopewa kuingia kidato cha kwanza mwaka.....katika Shule ya Sekondari  
ya Nangando na nitafika shuleni bila kuchelewa. Ninaahidi kwamba nitatii na  
kuzingatia sheria zote za shule na nchi. Nitakua mwanafunzi mwenye bidii katika  
masomo na kazi za elimu ya kujitegemea.

**B. KUTOSHIRIKI KATIKA MGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI**

Mimi ..... mwanafunzi wa kidato cha kwanza,  
Ninaahidi mbele ya mzazi/mlezi na familia yangu kwa ujumla, kuwa sitashiriki au  
kuchochea fujo, mgomo na makosa ya jinai kwa muda wote niwapo shuleni na  
nyumbani nitakuwa raia mwema na mzalendo kwa nchi yangu.

Saini ..... tarehe .....

Anuani yangu ya kudumu ni .....

**2. Sehemu ya mzazi/mlezi**

Mimi ..... ninakubali mtoto  
wangu ..... kusoma katika Shule ya Sekondari ya  
Nangando mwaka wa ..... Ninaahidi kumpatia mahitaji yote ya shule kama  
ilivyo katika maagizo ya kujiunga na shule. Aidha ninaahidi nitashirikiana na shule  
wakati wote kuona kuwa mwanangu anatekeleza wajibu wake kwa shule na taifa. Na  
nitafutilia maendeleo yake kitaaluma, tabia na mwenendo wa nidhamu ya mtoto  
wangu nikishirikiana na waalimu.

Anuani yangu ya kudumu ni .....

Namba ya simu.....

Iwapo nitapata uhamisho au kubadili makazi, ni lazima nitaijulisha shule kwa  
maandishi.

Saini ..... Tarehe.....

**KUMBUKA:** (Fomu hii irudishwe kwa Mkuu wa Shule ikiwa imejazwa)

## **MEDICAL EXAMINATION FORM**

Nangando Secondary School,  
P.O.Box 22,  
LIWALE.

To

THE MEDICAL OFFICER,

.....  
.....  
.....

Please examine.....

As to her fitness for pursuing further education at this school,

1. Haemoglobin .....
2. P.V. Bleeding .....
3. (a) Sight defect .....
- (b) Hearing.....
4. Blood Pressure.....
5. Urine for Sugar and Pregnancy test.....
6. Stool for routine examination.....
7. Asthma.....
8. Skin diseases.....
9. Leprosy .....
10. Epilepsy.....
11. Pulmonary tuberculosis.....
12. Deformity.....
13. Mental Problem.....
14. Comments.....

### **MEDICAL CERTIFICATE**

(To be completed by the Medical Officer)

I have examined the above named and consider that she/he is mentally and physically fit for studies.

**Signature .....**      **Date .....**

**Designation .....**      **Station .....**

**NB: (Fomu hii irudishwe Kwa Mkuu wa Shule ikiwa imejazwa)**